

## **A WARITHI KABLA YA KRISTO: WATUMWA (Wagalatia, 3: 26-29)**

- ❖ Je; Tulikuwaje warithi baada ya kuwa watoto chini ya Mwalimu?
  - Kama tulivyojifunza awali, sisi si watoto tena chini ya mwalimu baada ya kukutana na Yesu (fg. 25).
  - Tunakuwa wana na binti za Mungu (watu wazima) kwa Imani ndani ya Kristo —bila mwalimu (fg. 26).
  - Tunapobatizwa, tunamvaa Kristo (fg. 27).
  - Tu wamoja katika Kristo; rangi, madaraja ya kijamii na jinsi havidhuru tena (fg. 28).
  - Tunakuwa wana na biti wa Ibrahimu na warithi sawasawa na ile ahadi.” (fg. 29).

## **B WARITHI BAADA YA KRISTO: WAASILIWA (Wagalatia, 4: 1-3)**

- ❖ Kabla ya Yesu kuja, waisraeli kabla ya Yesu. Walikiwa “wakitumikishwa na kawaida za kwanza za dunia.” (fg. 3).
- ❖ hizo “kawaida” ni ABC, kanuni za msingi za Imani katika matinki hii. Ni sheria zilizokuwa kama walimu kwa waisraeli. Zilikuwa injili ya msingi, kivuli cha kile kilichokuwa kikija.

## **C MUNGU ALIMTUMA MWANAYE (Wagalatia, 4: 4)**

- ❖ Yesu alikuja dunia kama sehemu ya mpango wa mbingu uliotabiri, sio kwa bahati.
- ❖ Ingawa alikuwa ni Mungu, Alizaliwa na mwanamke. Aliuchukua ubinadamu wetu na kuwa mbadala halali, mwokozi wetu na Kuhani wetu mkuu.
- ❖ Alizaliwa chini ya sheria. Alitimiza matakwa ya sheria na kubeba adhabu yetu.
- ❖ Kwa kifo chake msalabani, alitimiza haki ya sheria, inayotaka kifo kwa mdhambi, hivyo kupata haki ya kuwakomboa wote wanaomwendea kwa Imani ya kweli na kujikabithi kwake.

## **D WALIOFANYIKA KUWA WANA NA BINTI (Wagalatia, 4: 5-7)**

- ❖ Yesu alitununua kwa gharama—Alitukomboa—, hivyo alituweka huru dhidi ya:
  - Ibilisi na hila zake (Ebr. 2:14-15).
  - Kifo (1Kor. 15:26-57).
  - Nguvu ya dhambi itutumikishayo (Rum. 6:22).
  - Hukumu ya sheria (Gal. 4:5)

## **E KURUDI UTUMWANI (Wagalatia, 4: 8-11)**

- ❖ Paulo aliwaonyesha Wagalatia faida zote za kuwa warithi wa Mungu kwa Imani katika Yesu, hivyo alishangazwa na wao kugeukia “kawaida” za imani. Kwa mujibu wa fungu la 10, waliamua kutunza:
  - Siku (Sabato za sikukuu).
  - Mwandamo mwenzi (mwezi mpya).
  - Majira (sikukuu za mwaka).
  - Miaka (Miaka ya sabato na Jubilee).
  - The years (the Sabbatical year and the Jubilee).
- ❖ Walikuwa warithi lakini walikataa kufanyika kuwa wana na kuwa watumwa tena.
- ❖ Ikiwa tuna uhusiano na Mungu uliojengwa katika sheria na kanuni pekee, tunakosa mbaraka wakuwa wana na binti za Mungu.